DeKalb County School District
Dkt. Devon Q. Horton, *Msimamizi*

Bw. Diijon DaCosta, Sr., *Mwenyekiti wa Bodi*
Bi. Deirdre P. Pierce, *Makamu Mwenyekiti*
Bi. Anna Hill
Bi. Whitney McGinniss
Bi. Allyson Gevertz
Bi. Vickie B. Turner
Dkt. Joyce Morley

**INAPASWA KUCHAPISHWA BILA KUKAWIA**

Tarehe 11 Novemba 2024

**Mawasiliano:**
Donald Porter, *Ed.D.* 678-481-4110
Carla Parker 404-734-1717

# Kaunti ya DeKalb Yatambua Shule 40 Zilizotunukiwa kama Viongozi wa Hisabati na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika katika Georgia

(STONE MOUNTAIN, GA)— Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (*DCSD*) inatangaza kwa fahari kwamba shule zake 40 zimetambuliwa na Idara ya Elimu ya Georgia kama Viongozi wa Hisabati na Viongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika kwa mwaka wa masomo wa 2023-2024. Heshima hii adhimu inaangazia kujitolea kwa Wilaya kwa ubora wa kimasomo na kujitolea kwa ufaulu wa wanafunzi katika hisabati na ujuzi wa kusoma na kuandika.

“Tunajivunia sana shule zetu 40 zilizotambuliwa kama Viongozi wa Hisabati na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika,” Msimamizi wa DCSD Dkt. Devon Q. Horton alisema. “Mafanikio haya yanaonyesha bidii ya wanafunzi wetu, kujitolea kwa walimu na wasimamizi wetu, na msaada wa ajabu kutoka kwa familia na washirika wa jamii yetu.

“Tunaposherehekea hatua hizi muhimu, tunatazamia ongezeko kubwa zaidi la ufaulu wa wanafunzi katika gredi zote. Kwa pamoja, tunaendelea kushirikiana ili kuimarisha taratibu zetu ambazo zinamwezesha kila mwanafunzi wa Kaunti ya DeKalb kufaulu kielimu na katika juhudi zao za siku zijazo.”

*Tuzo za Kiongozi wa Hisabati* hutuza shule kwa ufaulu au ukuaji wa kipekee katika hisabati. Katika Kaunti ya DeKalb, shule 24 zilitambuliwa kwa kuongeza asilimia ya wanafunzi waliopata alama katika kiwango cha Wanafunzi Stadi au juu zaidi katika mwaka wa 2023-2024 kwenye Tathmini za Georgia Milestones. Vigezo hivyo vinazingatia umuhimu wa ujuzi wa kuhesabu katika gredi za tano na nane, unaohitaji ukuaji wa juu kutoka kwa shule zilizo na viwango vya chini vya ufaulu. Tuzo za shule ya upili zinatokana na mitihani ya Mwisho wa Kozi ya Aljebra:  Miunganisho na Dhana.

| Jina la Mfumo | Jina la Shule | Tuzo za Kiongozi wa Hisabati |
|---|---|---|
| KAUNTI YA DEKALB | WYNBROOKE ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi (Gateway) wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | AUSTIN ELEMENTARY SCHOOL | Ufaulu wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 3; Ufaulu wa Gredi ya 4; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | DUNWOODY ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | MUSEUM SCHOOL AVONDALE ESTATES | Ukuaji wa Gredi ya 4; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | KITTREDGE MAGNET SCHOOL | Ufaulu Bora wa Gredi ya 4; Ufaulu Bora wa Msingi ya Gredi ya 5, Ufaulu Bora wa Gredi ya 6 |

| | | |
|---|---|---|
| KAUNTI YA DEKALB | WADSWORTH MAGNET SCHOOL | Ufaulu wa Gredi ya 4; Ukuaji wa Gredi ya 4; Ufaulu wa Gredi ya 6; Ufaulu wa Gredi ya 7; Ukuaji wa Gredi ya 7; Ufaulu Bora wa Msingi wa Gredi ya 8; Ufaulu Bora wa HS |
| KAUNTI YA DEKALB | GLOBE ACADEMY CHARTER SCHOOL | Ufaulu wa Gredi ya 7, Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 8 |
| KAUNTI YA DEKALB | TAPESTRY PUBLIC CHARTER SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 8 |
| KAUNTI YA DEKALB | ROBERT SHAW THEME SCHOOL | Ukuaji wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 4; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | CHAMBLEE MIDDLE SCHOOL | Ufaulu wa HS |
| KAUNTI YA DEKALB | TUCKER MIDDLE SCHOOL | Ufaulu wa HS |
| KAUNTI YA DEKALB | DEKALB ELEMENTARY SCHOOL OF THE ARTS | Ukuaji wa Gredi ya 4; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 8 |
| KAUNTI YA DEKALB | COLUMBIA ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | MCNAIR MIDDLE SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 8; Ufaulu wa HS |
| KAUNTI YA DEKALB | LIVSEY ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | WOODWARD ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | JOHN ROBERT LEWIS ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | ASHFORD PARK ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | CHESNUT ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | OAK GROVE ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | BRIAR VISTA ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | LAUREL RIDGE ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | RAINBOW ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | MONTGOMERY ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 5 |

*Tuzo za Kiongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika* huheshimu shule zinazoonyesha ufaulu au ukuaji wa kipekee katika umahiri au ustadi wa kusoma katika 2023-24. Katika Kaunti ya DeKalb, shule 16 zilitimiza sifa za kutambuliwa kama *Viongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika.* Vigezo vinalenga wanafunzi wanaosoma katika kiwango cha gredi au juu zaidi katika Tathmini za Georgia Milestones katika shule za msingi na za kati. Tuzo za shule za upili zinatokana na matokeo ya tathmini za Mwisho wa Kozi ya Fasihi ya Marekani.

| Jina la Mfumo | Jina la Shule | Tuzo za Kiongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika |
|---|---|---|
| KAUNTI YA DEKALB | AUSTIN ELEMENTARY SCHOOL | Ufaulu wa Msingi wa Gredi ya 3, Ufaulu wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | BARACK H OBAMA ELEMENTARY MAGNET | Ufaulu wa Msingi wa Gredi ya 3 |
| KAUNTI YA DEKALB | BRIARLAKE ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | BROWNS MILL ELEMENTARY SCHOOL | Ufaulu wa Msingi wa Gredi ya 3 |

| | | |
|---|---|---|
| KAUNTI YA DEKALB | CARY REYNOLDS ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 4 |
| KAUNTI YA DEKALB | DEKALB EARLY COLLEGE ACADEMY | Ufaulu wa HS |
| KAUNTI YA DEKALB | DEKALB ELEMENTARY SCHOOL OF THE ART | Ufaulu wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 4; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 6; Ufaulu wa Gredi ya 7; Ufaulu wa Gredi ya 8 |
| KAUNTI YA DEKALB | DEKALB SCHOOL OF THE ARTS | Ufaulu wa HS |
| KAUNTI YA DEKALB | INTERNATIONAL COMMUNITY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | KITTREDGE MAGNET SCHOOL | Ufaulu Bora wa Gredi ya 4; Ufaulu Bora wa Gredi ya 5; Ufaulu Bora wa Msingi ya Gredi ya 6 |
| KAUNTI YA DEKALB | LAUREL RIDGE ELEMENTARY SCHOOL | Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 5 |
| KAUNTI YA DEKALB | LEADERSHIP PREPARATORY ACADEMY | Ufaulu wa Msingi ya Gredi ya 6; Ufaulu wa Msingi ya Gredi ya 6; Ukuaji wa Gredi ya 7; Ukuaji wa Gredi ya 8 |
| KAUNTI YA DEKALB | PRINCETON ELEMENTARY SCHOOL | Ufaulu wa Msingi wa Gredi ya 3 |
| KAUNTI YA DEKALB | ROBERT SHAW THEME SCHOOL | Ufaulu wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Msingi wa Gredi ya 3; Ukuaji wa Gredi ya 4 |
| KAUNTI YA DEKALB | SHADOW ROCK ELEMENTARY SCHOOL | Ufaulu wa Msingi wa Gredi ya 3 |
| KAUNTI YA DEKALB | WADSWORTH MAGNET SCHOOL | Ufaulu Bora wa Gredi ya 4; Ufaulu Bora wa Gredi ya 5;Ufaulu Bora wa Msingi wa Gredi ya 6; Ufaulu Bora wa Gredi ya 7; Ufaulu Bora wa Gredi ya 8 |

Katika Jimbo lote, shule 624 zilitambuliwa kama Viongozi wa Hisabati, na shule 324 zilitunukiwa kama Viongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika.

Msimamizi wa Shule wa Jimbo, Richard Woods alipongeza shule zilizotunukiwa kama Kiongozi wa Hisabati na Kiongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika katika Georgia kwa kazi nzuri na mafanikio yao. Pia aliwapongeza kwa "kutekeleza Viwango vipya vya Hisabati vya K-12" na "kuleta mabadiliko makubwa katika ujuzi wa kusoma na kuandika."

**Viongozi wa Hisabati:** Bofya viungo vifuatavyo kwa orodha ya kina ya jimbo nzima ya Shule Viongozi wa Hisabati katika 2023-2024 na Vigezo vya Kiongozi wa Hisabati vya 2023-2024 MathVigezo vya Kiongozi wa Hisabati vya 2023-2024 Math.

**Viongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika:** Bofya viungo vifuatavyo kwa orodha ya kina ya jimbo nzima ya Shule Viongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika katika 2023-2024 na Vigezo vya Kiongozi wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika vya 2023-2024.

XXX